**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, SLP 113,Iselamagazi, SHINYANGA Simu/Fax: 0282-986382 Barua pepe: info@shinyangadc.go.tz
Website: www.shinyangadc.go.tz

***Unapojibu tafadhali taja:***
*Kumb.Na.SDC/C.4/7/Vol/52* *07.02.2024*

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga anawatangazia watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuomba nafasi za kazi zilizotajwa hapo chini, baada ya kupokea kibali chenye Kumb.Na.FA.228/613/01/066 cha tarehe 14.12.2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora.

### 1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III (NAFASI 3)

#### 1.1.1 SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha nne (IV) au Kidato cha sita (VI)
- Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada katika moja ya fani zifuatazo; Sheria,Elimu ya Jamii,Usimamizi wa Fedha,Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

#### 1.2.2 MAJUKUMU YA KAZI

(i) Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
(ii) Katibu wa Kamati ya Kijiji.
(iii) Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelewa na Halmashauri katika Kijiji.
(iv) Mshauri wa Kamati ya Kijiji Kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Kijiji.
(v) Msimamizi wa Utekelezaji wa Sheria ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Kijiji.

(vi) Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.

(vii) Msimamizi na Mtekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na Umaskini katika Kijiji.

(viii) Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi.

(ix) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

### 1.2.3 NGAZI YA MSHAHARA

- Ngazi ya Mshahara ni TGS B

### 1.2 DEREVA DARAJA LA II

### 1.2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV)
- Awe na leseni ya Daraja la C au E ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Cource) yanayotolewa na chuo cha VETA au NIT au Chuo kingine kinachotambulika na Serikali.

### 1.2.2 MAJUKUMU YA KAZI

(i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;

(ii) Kupeleka watumishi kwenye safari za kazi;

(iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari;

(iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali;

(v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari; na

(vi) Kufanya usafi wa gari.

**1.2.3 NGAZI YA MSHAHARA**

Ngazi ya mshahara ni TGS B.

**MASHARTI YAJUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini serikalini;

**ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;**

**iii.** Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.

iv. Waombaji ambao ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo,wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.

v. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminikapamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kuzaliwa,kidato cha nne,kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

**‘’Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates. - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI - Computer Certificate - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)’’**

**vii.** Testmonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**

viii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi waUmma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.

xi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

xii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 21 Februari, 2024.

Xiii **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa

pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA,**
**S.L.P 113.**
**SHINYANGA.**

*xiv Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielectroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anwani ifuatayo; http;portal.ajira.go.tz/(Anwani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal').*

Limetolewa na:

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA**